# TUJIFUNZE BIBLIA

## *SOMO LA 8*

### MAISHA MAPYA

Kabla mtu hajabatizwa anaamriwa na Mungu kutubu. Kutubu maana yake ni kuacha kutenda mabaya na kuanza kuzishika amri zote za Mungu. Basi, mtu akibatizwa bila kutubu dhambi zake atakuwa amejisumbua bure. Maana, Yohana ametuonya akisema:

"*Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki… kama yeye* (Mungu) *alivyo na haki; atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa bilisi hutenda dhambi tangu mwanzo… Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi nao. Mtu ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake.*" 1 Yohana 3:8,10

1. Hata ingawa mtu amebatizwa, lakini akiendelea kutenda dhambi yeye ni mtoto wa nani? _________________

Mtume Petro amesisitiza umuhimu wa kutubu dhambi akisema:

"*Atakaye kupenda maisha, na kuona siku njema, auzuie ulimi wake usinene mabaya, na midomo yake isiseme hila. Na aache mabaya, atende mema; atafute amani, aifuate sana. Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake husikiliza maombi yao; bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya.*" 1 Petro 3:10-12

2. Atakaye kuona siku njema auzuie ulimi wake usinene nini? _________________
3. Mtu huyo aache mabaya, atende nini? _________________
4. Uso wa Bwana ni juu ya nani? _________________

### MWENYE DHAMBI NI NANI?

Mwanadamu asidanganywe akifikiri kwamba yeye hana dhambi. Maana twasoma:

"*Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu.*" 1 Yohana 1:10

5. Tukisema kwamba hatukutenda dhambi twamfanya Mungu kuwa nani? _________________

### JE! TUZIFICHE DHAMBI?

Baadhi ya watu hudhani kwamba wanaweza kuficha dhambi zao Mungu asizione, Walakini Yesu alisema:

"*Hakuna neno lililositirika ambalo halitafunuliwa; wala lililofichwa ambalo halitajulikana na kutokea wazi.*" Luka 8:17

Tena, twasoma: "*Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.*" Mithali 28:13

6. Je! tunaweza kuficha dhambi zetu Mungu asizione? _________________

7. Mtu aungamaye dhambi zake, mbele ya Mungu na kuziacha atapata nini? _________________

Roho wa Mungu alimwongoza mtume Paulo kuwaonya watu wasiotaka kuacha dhambi zao akisema:

"*Kwa kadiri ya ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba, wajiwekea akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu, atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake… na wale wenye fitina, wasioitii kweli bali wakubalio dhuluma, watapata hasira na ghadhabu.*"

Warumi 2:5-6,8

8. Watu wasiotubu dhambi hujiwekea akiba gani? _________________

9. Watu wasioitii kweli watapata hasira pamoja na nini? _________________

**UTU WETU WA KALE UMEKUFA**

Katika somo la 6 tuliona mistari mingi sana inayothibitisha kwamba Yesu aliwaamuru watu wote kubatizwa kwa njia ya kutoswa majini. Kutoswa majini ni mfano wa kuzikwa kwake Yesu. Mungu amewaamuru wanadamu kubatizwa hivyo kusudi wafananishwe na Yesu. Maana katika kutubu na kubatizwa sisi nasi tunakufa! Eti! tunakufaje? Ni utu wetu wa ndani wenye dhambi ambao unakufa. Ebu! tuone neno la Mungu:

"*Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi <u>tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo</u> katika mauti yake… Kwa maana kama tulivyounganika naye <u>katika mfano wa mauti yake</u>, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; tukijua neno hili, ya kuwa <u>utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye</u>, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena.*" Warumni 6:2-6

10. Mungu ametuamnuru kubatizwa kwa kuzikwa (yaani, kutoswa) majini kwa sababu ubatizo huo umefananishwa na mauti ya nani? _________________

11. Katika ubatizo utu wetu wa kale wenye dhambi umefanya nin? _________________

Petro alisemna: "*Tangu sasa msiendelee kuishi katika tamaa za wanadamu, bali katika mapenzi ya Mungu, wakati wenu uliobaki wa kukaa hapa duniani. Maana wakati wa maisha yetu uliopita watosha kwa kutenda mapenzi ya Mataifa; kuenenda katika ufisadi, na tamaa, na ulevi, na karamu za ulafi, na vileo na ibada ya sanamu isiyo halali.*" 1 Petro 4:2-3

Paulo naye anazidi kutukumbusha kwamba ni lazima kuuua utu wetu wa kale. Paulo alisema:

"*Basi, vifisheni viungo vyenu viliyyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu: kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu. Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani, mlipoishi katika hayo. Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu. Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba.*" Wakolosai 3:5-10

12. Mkristo amevua utu wa kale pamoja na nini? ________________

Huko juu tuliambiwa kuuvua utu wa kale na kuuvaa utu mpya. Maneno hayo yanaonyesha kwamba kazi ya Mkristo si kuacha kutenda mabaya tu bali kazi yake ni kuanza kufanya mema badala ya mabaya. Yesu ametuonya kuhusu hatari ya kuyaondoa mabaya katika maisha yetu bila kuyajaza na mema. Alisema:

"*Pepo mchafu, amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika, asipate. Halafu husema, Nitarudi nyumbani kwangu nilikotoka; hata akija, aiona tupu, imefagiwa, na kupambwa. Mara huenda, akachukua pamoja naye pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza.*"

Mathayo 12:43-45

Ikiwa mtu huyo aliyetajwa na Yesu angalijaza maisha yake na mema, bila shaka yule pepo mchafu asingalipata nafasi ya kumwingia tena. Basi, kuondoa dhambi maishani mwetu hakutoshi bali ni lazima kujaza maisha yetu na matendo mema pia kusudi dhambi isiingie tena.

13. Je! inatosha kwa Mkristo kuyaondoa mabaya katika maisha yake bila kuanza kufanya mema?

________________

"*Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu.*" Wakolosai 3:12-14

"*Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.*" 1 Wakorintho 6:19-20

"*Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo; katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu. Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake.*" Wagalatia 5:19-24

14. Mtu anapobatizwa mwili wake huwa hekalu la nani? ________________

15. Katika miili yetu tumtukuze nani? ________________

16. Walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo gani? ________________

## MUNGU HANA UPENDELEO

Baadhi ya watu husema kwamba mwanadamu hawezi kuacha dhambi zake isipokuwa Mungu amemtaka aokolewe. Wanadhani kwamba Mungu huwanyima baadhi ya watu uwèzo wa kumshinda Shetani. Kwa sababu ya uongo huu watu wengi huendelea kutenda dhambi wakisema eti, Mungu hajawapa uwezo wa kutubu. Hivyo wanamshitaki Mungu wakidhani kwamba watakwepa hukumu hata ingawa hawajatubu. Lakini wamejidanganya, maana Petro alisema:

"*Hakika natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo; bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye.*" Matendo 10:34-35

"*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.*" 2 Petro 3:9

17. Je! Mungu ana upendeleo? _________________

18. Je! Mungu anataka mtu ye yote apotee? _________________

Kwa sababu Mungu hana upendeleo na kwa sababu hataki mtu ye yote kupotea ameahidi kwamba hatamwacha mtu ye yote ajaribiwe kupita uwezo wake. Neno la Mungu lasema:

"*Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.*" 1 Wakorintho 10:13

19. Mtu anapotenda dhambi, je! itakuwa halali kusema kwamba Mungu alimnyima nguvu za kutosha kushinda dhambi? _________________

## UPENDO WA MUNGU NA WOKOVU

Katika upendo wake, Mungu amewapa watu wote nafasi ya kuokolewa. Walakini Yeye hatamlazimisha mtu kuupokea wokovu. La! bali inatakiwa kwa kila mtu kujiokoa kwa kuyatii masharti ya Mungu yaletayo wokovu. Ndiyo maana Petro alihubiri siku ya Pentekoste akisema:

"*Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu… Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*" Matendo 2:38,40-41

20. Je! Petro aliwaambia watu kujiokoa wenyewe? _________________

"*Yohana amesema: Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hamgusi.* "1 Yohana 5:18

21. Je! ni kazi ya Mkristo kujilinda mwenyewe na dhambi? _________________

**TUJILINDEJE NA DHAMBI?**

Mtu akitaka kujiepusha na dhambi ni lazima ajilinde mawazo yake. Maana Yesu amesema:

"*Moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati, wivu, ushuhuda wa uongo, na matukano; hayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi.*" Mathayo 15:19

"*Mtu mwema katika akiba njema hutoa mema; na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya.*" Mathayo 12:35

Kwa hiyo, tumeambiwa: "*Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; maana ndiko zitokako chemchemi za uzima.*" Mithali 4:23

"*Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii.*" Warumi 8:5-7

"*Msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*" Warumi 12:1-2

22. Matendo mabaya hutoka katika moyo ulio na akiba gani? __________________

23. Mtu akitaka kuacha dhambi zeke ni lazima ageuzwe kwa kufanywa upya aini? __________________

Mistari hiyo inaonyesha hatari ya kusoma vitabu na magazeti maovu na kuzitazama sinema zisizofaa. Tena, ni hatari kufanya urafiki na watu waovu. Maana kwa kuona na kusoma na kusikia mambo maovu, mtu hujiwekea akiba mbovu moyoni mwake. Mungu ametuonya akisema:

"*Msidanganyike; mazungumzo mabaya huharibu tabia njema. Tumieni akili kama ipasavyo, wala msitende dhambi.*" 1 Wakorintho 15:33-34

24. Mazungumzo mabaya huharibu nini? __________________

25. Je! mtu, asomaye vitabu na magazeti maovu na kuzitazama sinema zisizofaa hujiwekea akiba njemna au akiba mbaya moyoni? __________________

Mtu ambaye hajilindi moyo wake na mawazo mabaya hataweza kumshinda Shetani. Basi, Mungu huwaambia Wakristo akisema: "*Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.*" Wakolosai 3:2

"*Mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.*" Wafilipi 4:8

Yohana ametuambia jinsi tunavyoweza kushinda dhambi. Alisema: "*Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu. Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu?*" 1 Yohana 5:4-5

Mtu akiamini kweli kweli kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu atajitahidi sana kuacha dhambi na kufanya mema kwa sababu zifuatazo: **(1)** atampenda Yesu na kutaka kumpendeza; **(2)** ataogopa hukumu; **(3)** atataka thawabu ambayo Yesu amewaahidi wale wanaomtii.

26. Yohana alisema kwamba kitu kinachoshinda ulimwengu ni nini? __________________

Huko juu tumesikia habari ya mambo mawili yanayotakiwa ili tushinde dhambi. Kwanza ni lazima kulinda mioyo yetu na mawazo maovu ya kidunia. Kisha, ni lazima kuijaza mioyo yetu na imani. Je! imani tutaipata wapi? Baadhi ya watu husema kwamba inatakiwa kuona ishara au miujiza kusudi mtu aweze kuwa na imani. Katika somo la 9 tutaongea kuhusu mambo hayo.

## MKRISTO NA MWILI WAKE

Mungu amesema: "*Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu, tena panoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu.*"

Isaya 57:15

27. Mungu anakaa na mtu aliye na roho iliyofanya nini? __________________

Paulo alisema: "*Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.*" 1 Wakorintho 3:16-17

"*Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vifaavyo. Vitu vyote ni halali; bali si vitu vyote vijengavyo… Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu.*"

1 Wakorintho 10:23,31

28. Mtu akiharibu mwili wake ambao ni hekalu la Mungu, Mungu atamfanyeje?

__________________

29. Hata katika chakula chetu na vinywaji vyetu lazima tumtukuze nani? __________________

30. Je! ni halali kwa Mkristo kutumia vileo, tumbako, na vitu vingine vinavyouharibu mwili wake?

__________________

"*Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye… Lo lote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadanu, mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi. Mnamtumikia Bwana Kristo.*"

Wakolosai 3:17, 23-24

31. Hata katika kazi ya kimwili Wakristo hawatumikii wanadamu bali humtumikia nani?

__________________

32. Mkristo akiwa kazini, je! imempasa kufanya bidii wakati mwenye mali yupo tu au hata asipokuwepo? __________________

"*Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai. Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.*" Yakobo 1:26-27

33. Je! Mkristo ajilinde na dunia pasipo nini? __________________

**AKIBA YA HAKI**

Watu fulani hudhani kwamba wanaweza kujiwekea akiba ya haki. Yaani, wanadhani kwamba ikiwa zamani walikuwa wakisali pamoja na Wakristo na kutoa fedha kwa kanisa, basi Mungu atawapokea mbinguni hata ingawa wameacha kufanya mambo hayo. Walakini Biblia yasema:

"*Mwenye haki atakapoghairi na kuiacha haki yake, na kutenda uovu, na kufanya machukizo yote kama yale afanyayo mtu mwovu, je, ataishi? Katika matendo yake yote ya haki aliyoyatenda halitakumbukwa hata mojawapo. Katika kosa lile alilolikosa, na katika dhambi yake aliyoitenda, atakufa.*" Ezekieli 18:24

34. Je! mtu ataweza kuingia mbinguni kwa sababu ya matendo yake mema aliyoyatenda zamani ikiwa ameacha kuyafanya? __________________

Yesu alisema: "*Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.*" Ufunuo 2:10

************************************************************************************

Jina lako …………………………………………………
Anwani yako ……………………………………………

***KANISA la KRISTO***
***Tanzania***